

HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA
MUHTSARI WA KIKAO CHA DCC KILICHOFANYIKA TAREHE
03/10/2016 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA

WALIOHUDHURIA

- | | |
|-----------------------------------|------------------------|
| 1. MH. LT. CLO. MICHAEL MNTENJELE | MWENYEKITI (DC) |
| 2. BW. AIDAN J. BAHAMA | KATIBU (DED) |
| 3. BW. VEDASTUS TIBAIJUKA | DAS |
| 4. MH. ERICK E. NKILAMACHUMU | M/KITI WA HW (DIWANI) |
| 5. MH. WILBARD BAMBARA | M/M/KITI WA HW(DIWANI) |
| 6. ASKOFU SEVERINE NIWEMUGIZI | MJUMBE |
| 7. BW. DAVID BUKOZO | MAT |
| 8. MH. JOHN SHIM'IMANA | DIWANI-KIBIMBA |
| 9. MH. GWIHANGWE M. EDWARD | DIWANI-NGR-MJINI |
| 10. MH. GWASSA NTUNGIYE | DIWANI-NYAMIAGA |
| 11. BI. ELIZABETH MICHAEL | TCRS |
| 12. MH. JACOB SENTORE | DIWANI-KIRUSHYA |
| 13. BW. STEPHEN RUNZANGA | M/KITI NGARA FARMERS |
| 14. MH. SAFARI M. BANIGWA | DIWANI-MABAWE |
| 15. MH. ROMAN MITABARO | DIWANI-KEZA |
| 16. MH. MKUBILA S. SOUD | DIWANI-M/SAGAMBA |
| 17. MH. SAID R.SOUD | DIWANI-KABANGA |
| 18. BW. IMANI RICHARD | A/USTAWI WA JAMII |
| 19. MH. ZAWADI A. COASMAS | DIWANI-VITI MAALUMU |
| 20. MH. JOHN E. RUZIGE | DIWANI-NTOBEYE |
| 21. MH. PHILBERT M. KIIZA | DIWANI-KASULO |
| 22. MH. HAMIS B. HAMADI | DIWANI-RULENGE |
| 23. MH. NZEYE LEONARD | DIWANI-MUGANZA |
| 24. MH. EDITHA MWINULA | DIWANI- VITI MAALUMU |
| 25. BW. ERICK ELIAZARY | WEO-RULENGE |
| 26. BW. YOTHAMU JOHN | WEO KEZA |
| 27. BW. SLYVESTER MAKUMBA | WEO-NYAKISASA |
| 28. BW. GOZIBERTI ONESMO | KATIBU ACT WAZALENDO |
| 29. BW. JAMES | M/KITI ACT WAZALENDO |
| 30. BI. BETTY S. MUNUO | A/ARDHINA MALIASILI(W) |
| 31. BW. SIMEON NDYAMUKAMA | K.N.Y MHANDISI WA MAJI |
| 32. BW. BURILO E. DEYA | MWANASHERIA(W) |
| 33. BW. BIGAMBO AMOS | AFISA MIPANGO(W) |

34. BW. JULIUS ERENEST	K/DO-NYAMIAGA
35. BW. JONAS J. GWASSA	WEO-MABAWE
36. BW. PASTORY MSABILA	DO-M/SAGAMBA
37. BW. JAWADU YUSUPH	DO-KANAZI
38. BW. WILFRED MAGIGE	DCSQA (W)
39. BW. MICHAEL NDYAMUKAMA	KATIBU TSD(W)
40. BW. SABUNI S. KASUBI	Ag. DE(W)
41. BW. TOBA A. MHINA	DEMO/TEO NGR- MJINI
42. BW. COSTANTINE MUDENDE	Ag. DAICO(W)
43. BW. SANGATATI J	DLFO (W)
44. MH. VAILETH MADENDE	DIWANI-VITI MAALUMU
45. MH. SUZANA B. NJOJOLI	DIWANI- VITI MAALUMU
46. BW. REVOCATUS NDYEKOBORA	DMO(W)
47. BW. OWDEN MBUBA	DHRO(W)
48. BW. MARTON JAMES	Ag. DSEO (W)
49. BW.FREDRICK KAKURU	Ag. EO
50. BW. MASOUD B.A	DT(W)
51. BW. KEFA	
52. MH. REHEMA S. RAMADHANI	DIWANI-VITI MAALUMU
53. MH. GEORGIA MNYONYERA	DIWANI-VITI MAALUMU
54. BI. SAKINA CHAMITI	MRATIBU TASAF(W)
55. BW. CHRISTOPHER NZOYA	WEO-MUGOMA
56. BW. RUKIZA ABEID	ICTO
57. BW. HASSAN B. ALLY	WEO-NGARA-MJINI
58. BW. ZACHARIA MESKIAD	WEO-KABANGA
59. BW. SELEMAN MESHACK	M/KITI CWT(W)
60. MCH. FRANCIS JACOB	KANISA LA PEFA
61. BI. PALITHA CLEOPHAS	SW
62. BW. MARWA K	DIO
63. BW. MASATU B	SW
64. BW. MORIS MOMBIA	Ag. DO-RULENGE
65. BW. BENETH M. RUSULE	WEO-KIBOGORA
66. BW. KAKURU N. RUBAMBURA	VEO-RUGANZO
67. BW. JUSTA KAGIMBO	TTCL-NGARA
68. MH. LAURENT JOHN	DIWANI-NYAMAGOMA
69. BW. LAURENT GERVAS	MWANDISHI WA HABARI
70. MH. ADRONIZI BURINDOLI	DIWANI-KIBOGORA
71. BW. COSMAS J	WEO-M/SAGAMBA
72. BW. ALEX MULENGELA	WEO-BUKIRIRO
73. BW. ISACK NICODEMU	WEO-MUGANZA

74. BW. MOSES KICHOGO
75. BW. EZEKIEL ZEPHANIA
76. BI. REHEMA WILLIAM
77. BW. PETER KAPALALA
78. BI. REINFRIDA ANZIGARY

ICO
WEO-BUGARAMA
REDIO-KWIZERA
WEO-KASULO
CC (H/W)

Katibu alianza kwa kuwasalimia wajumbe na kumkaribisha Katibu Tawala aweze kumkaribisha Mwenyekiti kwa ajili ya kufungua kikao, aidha alieleza kwanza kikao cha DCC ni vyema kiwe kinatangazwa katika Redio- Kwizera ili kila mwananchi aweze kupata taarifa. Katibu Tawala aliwasalimia wajumbe na kumkaribisha Mwenyekiti. Mwenyekiti aliwasalimia wajumbe na kuwakaribisha katika kikao pia aliwaomba wajumbe kuchangia katika agenda zilizowasilishwa katika kikao pia kueleza changamoto mabazo kama Wilaya inakutana nazo. Kikao kilifunguliwa saa 4.40 asubuhi.

MUHT NA 2/2016/2017: KURIDHIA AGENDA

Mjumbe mmoja alieleza kwamba katika kujadilia agenda ya kudhibiti wanafunzi hewa katika taarifa hakuna kiambatanisho kilichowasilishwa katika ukurasa wa 8. Baada ya majadiliano Wajumbe walipokea agenda na kuridhia.

MUHT NA 3/2016/2017: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA

Katibu Tawala alisema kwamba Muhtasari huu hauna maazimio ya kikao kilichopita

MUHT NA 4/2016/2017: TAARIFA YA HALI YA UTENGENEZAJI WA MADAWATI

Afisa Elimu Msingi aliwasilisha taarifa na kueleza kwamba kulikuwa na uhitaji wa madawati 24609 madawati yaliyokuwepo yalikuwa 15686 hivyo kuwepo na upungufu wa madawati 8923

Aidha Afisa Elimu Msingi alieleza mikakati iliyowekwa ili kufanikisha utengenezwaji wa madawati

1. **Kushirikisha Kamati za Maendeleo za Kata (WDC)**, mkakati huu unalenga kukamilisha madawati kulingana na mahitaji ya kila shule zilizoko katika kata hisika. Lengo lilikuwa ni kukamilisha madawati 2793
2. Kukarabati madawati mabovu yaliyokuwepo shuleni , ukarabati wa madawati mabovu unatekelezwa kwa kutumia fedha za matumizi ya kawaida ya shule (fungu la ukarabati), lengo lilikuwa kukarabati madawati 1800.
3. Kutumia fedha zinazopatikana katika Halmashauri, Katika mkakati huu Wilaya ilianza kutumia Tshs. 29,676,910/= za Idara ya Elimu Msingi kutengeneza madawati 500. Fedha hizi zilitumika katika kununulia square pipes 1250 na kupasua mbao 1000, mafuta yakusomba mbao na gharama za ufundi wa madawati 500
4. Kuhamasisha jamii kuchangia madawati, katika mkakati huu wananchi, wadau wa maendeleo wamechangia kwa hiari kupitia mikutano ya harambee iliyokuwa

inaendeshwa na Mkuu wa Wilaya katika meneo ya Ngara Mjini, Benaco-Kasulo, Murusagamba, Kabanga, Rusumo na Mugoma. Kupitia harambee hiyo zilikusanywa jumla ya Tshs. 24,252,000/=. Aidha kupitia mkakati huu Wakuu wa Idara, Waheshimiwa Madiwani walichangia dawati moja kila mmoja na Watumishi walichangia Tshs. 5000/= au ubao wa futi 12 wenye thamani ya Tshs. 5000/=

Hali ya madawati kufikia tarehe 29/09/2016 utengenezaji wa madawati upo chini ya Kata na Wilaya. Kwa ngazi ya kata walitakiwa kutengeneza madawati 5170 na ngazi ya Halmashauri madawati 3753

Afisa Elimu Msingi alieleza kwamba pamoja na mafanikio ya kukamilisha matengenezo ya madawati, zipo Changamoto kama vile Halmashauri inakabiliwa na deni la Tshs.114,000,000/= gharama za kulipia ufundi na Tshs. 58,973,993/= kama gharama za ununuzi wa square pipes. Wajumbe walipokea taarifa na kujadili;

Mjumbe mmoja alihoji juu ya mikakati iliyowekwa ili kuweza kulipa deni la Tshs. 114,000,000/= ambalo Halmashauri inadaiwa na mikakati ya upatikanaji wa fedha za ununuzi wa square pipes.

Afisa Elimu Msingi alisema kwamba Halmashauri inaendelea kujikopesha fedha ili kupunguza madeni ya ufundi, aidha alieleza kwamba kuna fedha Tshs. 198,000,000/= ambayo ilitengwa kwa ajili ya utengenezaji wa madawati kwa mwaka wa fedha 2016/2017, hivyo pindi fedha hizo zitakapoletwa zitapelekwa kulipa madeni moja kwa moja.

Katibu Tawala (W) alihoji juu ya ahadi zilizotolewa na wananchi kama fedha zinafuatiliwa na kukusanywa ili zitumike katika kupunguza madeni, pia alihoji juu ya ahadi iliyotolewa na Benki ya NMB kama tayari walishatengeneza madawati waliyoahidi.

Afisa Elimu msingi alijibu kwamba anaendelea kuwakumbusha kwa kuwapigia simu wale wote waliotoa ahadi zao aidha alieleza kuna changamoto ya kutopata ushirikiano toka kwa wahusika. Ahadi zilizotolewa na Benki ya NMB alimuomba Mwenyekiti wa Halmashauri pamoja na Mkurugenzi Mtendaji kumsaidia katika kufuatilia kwa sababu Benki ya NMB iliahidi kutengeneza madawati na sio kutoa fedha.

AZIMIO: Mkurugenzi Mtendaji afuatilie ahadi iliyotolewa na Benki ya NMB na majibu yatakayotolewa na Benki ya NMB yawasilishwe kwa Mwenyekiti wa Halmashauri na taarifa itatolewa kupitia vikao vya Halmashauri.

Mjumbe mmoja alisema kwamba kwa ahadi ambazo zilitolewa na Wana Ngara waishio Dar es Salaam, pindi watakapoleta fedha wanataka kuona madawati yaliyotengenezwa kupitia ahadi zao yanawekwa nembo ya chama chao.

Mjumbe mmoja alishauri Afisa Elimu Msingi kuwasiliana na Watendaji wa Kata ili kupata takwimu sahihi ya madawati yanayotengenezwa kupitia ngazi ya Kata.

Afisa Elimu Msingi alisema kwamba kuhusu takwimu, kuna takwimu zinazotolewa na Maafisa Tarafa ambazo ni takwimu za ujumla juu ya matengenezo ya madawati na takwimu ambazo zinatolewa na Watendaji wa Kata hivyo kama Halmashauri inaweza kuwa na takwimu za aina 2, aliwaomba Maafisa Tarafa kutoa takwimu za madawati yanayotengenezwa kila wiki.

Mjumbe mmoja alisema kwamba alipita katika maeneo ambayo madawati yanatengenezwa na kugundua kuwa matengenezo ya madawati yamesimama na alipojaribu kuhoji alielezwa kwamba mafundi bado wanadai fedha kwa ajili ya matengenezo ya madawati.

Katibu alisema kwamba alishasaini Hundi ya Tshs. 30,000,000/= kwa ajili ya kulipa mafundi pia alipohudhuria kikao cha ALAT, Waziri Mkuu Mh. Kassim Majaliwa Majaliwa aliahidi kutoa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Wajumbe walitaka kupata ufafanuzi kama mbao zinazotengeneza madawati zinatibiwa, Afisa Elimu Msingi alieleza kwamba kuhusu kutibu mbao za madawati mwanzoni waliweka bajeti kwa ajili ya kutibu mbao lakini ilionekana kuwa gharama za kutibu mbao ni kubwa hivyo waliona ni vyema kutumia fedha katika matengenezo ya madawati.

Mwenyekiti wa Halmashauri alisema kwamba utengenezaji wa madawati una changamoto ya upatikanaji wa miti, aidha alishukuru kuwepo kwa msitu wa Buseke ambao umesaidia sana katika matengenezo ya madawati, alishauri Waheshimiwa Madiwani kusimamia katika suala zima la utengenezaji wa madawati katika Kata zao, aidha alitoa angalizo kuwa madawati yanatengenezwa kwa kasi lakini haijulikani ni wapi madawati haya atahifadhiwa, aliwaomba wajumbe kuanza kuandaa vifaa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa hivyo kila kiongozi ajipande katika kuandaa vifaa

Mwenyekiti alisema kwamba Watendaji wa Kata katika maeneo yao wahakikishe wanakamilisha majukumu yao ikiwemo katika suala zima la matengenezo ya madawati.

MAAZIMIO:

1. Afisa Elimu Msingi afuatilie ili utengenezwaji wa madawati ukamilike
2. Afisa Elimu Msingi afanye ufuatiliaji ili kutambua idadi ya madawati yaliyotengenezwa katika ngazi ya Kata ili kubaini madawati yaliyotengenezwa katika ngazi ya Kata na ngazi ya Wilaya

MUNT NA 5/2016/2017: MIKAKATI YA KUONDOA WANAFUNZI HEWA KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI

Afisa Elimu Msingi aliwasilisha taarifa husika kuhusu wanafunzi hewa walioko katika shule za msingi na sekondari, aidha alieleza kwamba Idara imekwa ikifanya uhakiki wa wanafunzi ili kudhibiti uwepo wa wanafunzi hewa, utaratibu uliotumika ni kama ufutao;

- i. Kupitia daftari za mahudhurio kwa kila shule
- ii. Kujaza takwimu za wanafunzi kama walivyokuwa kwenye mfumo wa TAMISEMI (BEMIS) kama zilivyokuwa tarehe 31/03/2016
- iii. Kulinganisha takwimu zinazoleta fedha toka mwaka 2015/2016 na takwimu zilizopo kwa mwaka 2016/2017

Kupitia takwimu hizo wamebaini kuwa;

1. Wanafunzi 62868 wanaletewa fedha tangu mwaka 2015/2016
2. Kupitia daftari la mahudhurio ya kila shule Idara imebaini kuwepo kwa wanafunzi 71914 yaani wavulana 35897 na wasichana 36017

Kupitia Waratibu wa Elimu Kata baada ya kuhesabu wanafunzi kwa kila shule walibaini kuwepo kwa wanafunzi 70826 wavulana 35370 na wasichana 35456

Mikakati ya kudhibiti wanafunzi hewa ilikuwa kama ifuatavyo;

- i. Kuhesabu wanafunzi wote walioko mashuleni
- ii. Katika kufanya uhakiki ilibainika kuwepo kwa wanafunzi hewa katika shule za msingi Rulenge, Kumugamba, Kanyinya, Ruhuba, Rulama, Kumubuga, Kumwendo, Kahama, Murugunga, Nyamiaga na Buhororo.
- iii. Kupekua kumbukumbu nyingine za shule hasa “Admission Register”
- iv. Kuchukua hatua stahiki kwa yeyote atakayehusika kusababisha kuwepo kwa wanafunzi hewa

Aidha katika shule za sekondari 29 zilizoko katika Wilaya ya Ngara kati ya hizo shule za sekondari 23 zinamilikiwa na Serikali na shule za sekondari 6 zinamilikiwa na watu binafsi, aidha shule zinazomilikiwa na serikali zina jumla ya wanafunzi 7456 ikiwa wavulana ni 3800 na wasichana 3656.

Mikakati ya kudhibiti wanafunzi hewa shuleni;

- i. Kuwafukuza wanafunzi watoro wa kudumu kupitia vikao vya bodi za shule
- ii. Kufuatilia na kudhibiti uwepo wa wanafunzi shuleni kwa kufanya ukaguzi wa ana kwa ana
- iii. Kutoa elimu kwa Wakuu wa shule na waalimu wa Takwimu kuhusu uandaaji, uchambuzi na utoaji wa takwimu halisi wakati wa ujazaji wa takwimu za shule

- iv. Kupanga bajeti kulingana na wanafunzi waliopo na sio waliopangwa kujiunga na masomo kwa mwaka husika kwa sababu sio wote watakaopangwa watawezakuripoti shuleni kwa ajili ya usajili
- v. Kuhimiza na kufuatilia kuripoti kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza na kidato cha tano kwa 100%
- vi. Kuwachukulia hatua Wakuu wa shule na walimu wote watakaotoa takwimu za wanafunzi zisizo sahihi.

Wajumbe walipokea taarifa na kuijadili kama ifuatavyo;

Mjumbe mmoja alisema kwamba Afisa Elimu Msingi alitoa taarifa kwamba kuna waraka wa kuunda kamati mpya za shule na waraka ulitolewa tarehe 30/08/2016 na ilitakiwa kamati hiyo kuwa na wajumbe 5 ambao kati yao ni wazazi, alitaka kufahamu kama utaratibu ulitolewa unafaa kwa sababu waalimu wakuu walichelewa kupata waraka na kushindwa kufanya vikao na wazazi ili kufanya uchaguzi wa wajumbe wa kamati ya shule, je Afisa Elimu Msingi haoni kwamba walimu wakuu wanaweza kutoa taarifa ambazo sio sahihi

Mwenyekiti wa Halmashauri alisema kwamba kwa Kata ya Bukiriro waraka huo ulishafika na walifanikiwa kufanya mkutano na wazazi na kuchagua wajumbe wa kamati za shule , aidha alitoa angalizo kwamba alipohudhuria kikao cha ALAT ilitolewa taarifa ya kuwepo kwa wanafunzi hewa katika mashule na kuutaja Mkoa wa Arusha kwamba kuna Wilaya ina wanafunzi hewa lakini haikutajwa ni Wilaya gani.

Aidha ilielezwa kwamba kumekuwepo na tabia ya waalimu kuweka majina ya wanafunzi ambao hawako shuleni ili kuweza kupata fedha za ruzuku zinazoletwa na Serikali.

Mwenyekiti wa Halmashauri alieleza kwamba Waratibu wa Elimu Kata hawakai katika vituo vyao vya kazi hivyo kupelekea utoaji wa taarifa za uongo, Afisa Elimu Msingi asaidiane na Afisa Utumishi kuhakikisha Waratibu Elimu Kata pamoja na Watendaji wa Kata kuishi katika vituo vyao vya kazi.

Mjumbe alisema kwamba kumekuwa na tabia ya Wajumbe wa Bodi za shule kutohudhuria vikao kwa sababu hakuna posho, hii inapelekea Wakuu wa shule kutoa taarifa ambazo sio sahihi.

Mjumbe alisema kwamba zilitolewa siku 90 ambapo kama mwanafunzi hajahudhuria shuleni afutwe, alishauri iwekwe mikakati mizuri kabla ya wanafunzi hao kufutwa.

Mjumbe mwingine alishauri wazazi kufuatilia watoto wao kama wanahudhuria shuleni ili kupunguza wanafunzi hewa.

Mjumbe mmoja alisema kwamba kuna wanafunzi ambao wana magonjwa sugu, alishauri Afisa Elimu Msingi afuatile na ikiwezekana wanafunzi hawa wafutwe.

Mjumbe mwingine alishauri kwamba ili Halmashauri iweze kuendelea kielimu Afisa Elimu Msingi apitie mara kwa mara katika shule na kuona hali halisi iliyopo, alishauri kuwatumia Waratibu wa Elimu Kata ili kuweza kupata takwimu sahihi za idadi ya wanafunzi walioko shuleni.

Katibu Tawala alisema kwamba tatizo la kuwepo kwa wanafunzi hewa pia Inajadiliwa katika vikao vya ulinzi na usalama hivyo Mkurugenzi Mtendaji amuagize Afisa Elimu msingi kupeleka taarifa ya wanafunzi hewa kwa Mkuu wa Wilaya , pia aliomba waraka wa kuanzisha kamati mpya za shule uliotolewa Afisa Elimu Msingi azalishe na kuwagawia wajumbe

Mwenyekiti alisema kwamba kilifanyika kikao chaWakuu wa shule na waliagizwa kutoa takwimu sahihi na pia Bodi za shule zisiwe mahali pa kuweka saini tu, Bodi za shule zinatakiwa kufanya vikao na pia ufanyike ufuatiliaji wa makini juu ya wanafunzi walioko mashuleni pia kufuatilia takwimu zinazotolewa na Waalimu wakuu.

Aidha Afisa Elimu Msingi alifafanua juu ya kuwepo kwa utofauti wa takwimu na fedha zinazotolewa na Serikali, alieleza kwamba fedha zilizoletwa ni za bajeti ya mwaka 2014/2015, Afisa Elimu Msingi alieleza hatua zilizochukuliwa katika shule zilizobainika kuwa na wanafunzi hewa kuwa ni pamoja na kuwaandikia barua Waalimu wakuu waweze kujieleza kwanini walitoa takwimu za uongo, pia Afisa Elimu Msingi anaendelea kufuatilia.

Katibu alisema kwamba ilitolewa fomu maalumu ambayo kila shule inatakiwa kutoa takwimu zilizo sahihi na Mkuu wa shule atatakiwa kusaini yeye pamoja na Mratibu wa Elimu kata na kukubali kuwa takwimu zilizotolewa ni sahihi na kuwasilishwa kwa Mkurugenzi Mtendaji na endapo itagundulika kuwa takwimu zilizotolewa sio sahihi Mwalimu Mkuu atawajibishwa.

Mdhibiti ubora wa shule alisema kwamba walipitia mahudhurio na daftari la uandikishaji wanafunzi toka darasa la kwanza mpaka darasa la 7 na takwimu iliyotolewa ya wanafunzi walioko shuleni ndiyo hiyo iliyowasilishwa katika kikao, pia ilionekana kuwepo kwa utoro uliokithiri katika darasa la 6 na kama vile darasa hilo halipo.

MAAZIMIO:

1. Afisa Elimu Msingi na Afisa Elimu Sekondari wafuatilie ili kbaini wanafunzi hewa na kutoa taarifa kwa Mkuu wa Wilaya kwa ajili ya kuchukua hatua.
2. Afisa Elimu Msingi na Afisa Elimu Sekondari wafuatilie ili wajumbe wa Bodi waliomaliza muda wao wachaguliwe wengine aidha vikao vya Bodi vifanyike kulingana na maelekezo yaliyopo.

3. Halmashauri ya Wilaya ya Ngara iige mfano toka katika Halmashauri nyingine ili kuanzisha Mfuko wa Elimu wa Wilaya ya Ngara.

MUHT NA 6/2016/2017: MAANDALIZI YA KILIMO (MSIMU WA KILIMO)

Afisa Kilimo aliwasilisha taarifa ya malengo ya uzalishaji na matarajio kwa mwaka 2016/2017 kulima jumla ya Hekta 64,940 na kupata mavuno ya Tani 437,263.24 za mazao mchanganyiko lakini pia Idara inatarajia kutekeleza miradi ifuatayo, Kahawa, Mahindi, Maharage, Parachichi, Nanasi na viazi vitamu, pia Watendaji wa Katawanatakiwa kuhakikisha kila kaya inakuwa na ekari zisizopungua 2. Wajumbe walipokea taarifa na kuijadili.

Mjumbe mmoja alisema kwamba Afisa Kilimo alieleza kuwa Wakulima wawatumie Wataalamu walioko vijijini, alitaka kufahamu wakulima watawafahamu vipi pia Wataalamu wa ugani hawatoshi, pia walishaazimia katika kikao kilichopita uzalishaji wa mazao mengine uongezwe kama vile alizeti, tangawizi na mengineyo, aidha alishauri kwamba Afisa Kilimo atoe matangazo ya wapi mashine za kusindika alizeti zinapatikana na hata zilizosimikwa tayari bado hazifanyi kazi.

Mjumbe mwingine alisema kwamba Wataalam wa ugani hawawatembelei wakulima pia Afisa Kilimo ana mikakati gani katika kuanzisha kilimo cha mazao kama vile alizeti kwa sababu kama mbegu za alizeti zitaletwa wananchi wapo tayari kununua na kulima zao hilo.

Mjumbe mmoja alisema kwamba Afisa Kilimo angetoa elimu ya namna ya kuhifadhi mazao kwa sababu kuna baadhi ya mazao yasipohifadhiwa vizuri yanaharibika haraka

Mjumbe mwingine alisema kwamba kwa Wilaya ya Ngara anashauri Idara ya Kilimo kupokea ushauri unaotolewa na wakulima, pia baadhi ya Kata zipo katika mpango wa ruzuku ya pembejeo za kilimo alishauri pembejeo kuletwa kwa wakati na sio baada ya msimu wa kilimo.

Katibu Tawala alisema kwamba Waheshimiwa Madiwani ni viongozi katika Kata zao hivyo wasimamie suala zima la wanachi kufanya kazi na kuacha kunywa pombe katika masaa ya kazi, alishauri Idara ya Kilimo kutoa elimu hasa katika magonjwa kama vile unyanjano na pia kuandaa mikakati ya kukabiliana na janga la ukame ambao unaweza kujitokeza wakati wowote.

Mwenyekiti alisema kuhusu suala la pembejeo Idara ya Kilimo inapata maelekezo toka ngazi za juu, aliomba suala la pembejeo kwenda kujadiliwa katika kikao cha RCC, aidha aliongeza kwamba Idara ya Kilimo iandae mpango wa kuandaa maghala ya kutunzia mazao pia ipo haja ya kuhamasisha wananchi kulima mazao ya biashara kama vile alizeti,

tangawizi na mengineyo, aliwaomba Waheshimiwa Madiwani kufanya ufuatiliaji kwa wananchi na kuwaeleza kuwa wanatakiwa kufanya kazi katika masaa ya kazi na sio kwenda katika vilabu vya pombe.

Mjumbe mmoja alishauri kwamba iwekwe mikakati ambapo kila kaya iwe na miche isyopungua 10 kwa ajili ya kilimo cha parachichi, pia alieleza kwamba kuna vifaa vya kupandia ambavyo vilinunuliwa kwa gharama kubwa lakini havitumiki na vimehifadhiwa stoo, alishauri wakulima wangeelimishwana kuweza kutumia vifaa hivyo kwa ajili ya kupandia mazao.

Afisa Kilimo alisema kwamba takwimu zote za masuala ya kilimo zinatoka katika Kata kupitia katika vikao vya WDC vya mwezi wa Julai kwa ajili ya kuandaa mpango, mashine za kutengeneza mafuta ya alizeti zilijengwa kupitia mradi wa CONCERN ambapo REDESIO walipewa kazi ya kusimika mashine hizo, lakini jambo hilo wananchi wengi hawalifahamu kwa sababu bado mashine hizo hazijakabidhiwa kwa Halmashauri

Aidha alieleza kwamba ili Wataalam waweze kuwafikia wakulima, ilishauriwa wakulima wajiunge katika vikundi ili Mtaalam anapokuja aweze kutoa elimu kwa pamoja. Mifuko ya kutunzia mazao ipo na imehakikiwa tatizo lipo katika kufunga mifuko hiyo kwa sababu wakati wa kufunga mkulima anatakiwa ahakikishe hewa haipiti katika mfuko kwa kufunga mfuko uliokuwa ndani kwanza na kumalizia mfuko wan je na mazao yanatunzwa bila kuharibika kabisa, pia dawa za kuzuia wadudu hazipo katika Idara ya Kilimo alishauri wakulima kununua dawa katika maduka ya pembejeo za kilimo.

Suala la pembejeo bado kama Idara ya Kilimo haijapata maelekezo toka ngazi za juu kama zitaletwa ama la, alishauri wakulima kununua pembejeo katika maduka ya madawa ya pembejeo, pia endapo pembejeo zitaletwa wakulima wasisite kuzichukua kwa ajili ya kuzitumia katika msimu ujao wa kilimo.

MAAZIMIO:

1. Kikao cha DCC Ngara kinaomba kupitia kikao cha kinachofuata kufuatilia suala la pembejeo za kilimo kuletwa kwa wakati kwa wakulima kulingana na misimu ya kilimo iliyoko katika Wilaya ya Ngara kuanzia mwezi Julai kila mwaka.
2. Afisa Kilimo awaagize Maafisa Kilimo kuondoka maofisini na kwenda kwa wananchi ili kutoa ushauri, maelekezo na Teknolojia mpya ya kilimo.

MUHT NA 7/2016/2017: MIKAKATI YA MAKUSANYO YA NDANI

Mweka hazina aliwasilisha taarifa ya mikakati ya makusanyo ya ndani kuwa

- i. Kufanya uhibitaji wa mara kwa mara wa mapato katika maeneo mbalimbali ya kukusanyia mapato

- ii. Kutunza Kumbukumbu za makusanyo ya mapato kupitia mfumo wa Data base
- iii. Kufanya ukaguzi wa kushtukiza katika vyanzo vya mapato katika Kata/ Kijiji
- iv. Kuwachukulia hatua za kisheria watu wanaogoma au kushawishi wengine kugoma kulipa ushuru.
- v. Kuhakikisha vitendea kazi vya shughuli za kufuatilia na kukusanya mapato vinapatikana kwa mudamuafaka kama vile mafuta, gari risiti za kukiri mapokezi ya mapato na posho za muda wa ziada.
- vi. Kutoa elimu kwa jamii ya kuona umuhimu wa kulipa ushuru wa biashara
- vii. Ushirikishwaji wa kila Mtumishi wa kila Idara kuwajibika katika ukusanyaji wa mapato.
- viii. Kupata ushirikiano toka katika Taasisi zinazohusiana na zoezi la ukusanyaji wa mapato.

Wajumbe walipokea taarifa na kuijadili kama ifuatavyo;

Mjumbe mmoja alisema kwamba ni kweli vifaa vya kukusanyia mapato vilishatolewa mfano katika Kata ya Rulenge lakini changamoto ipo katika 10% inayotakiwa kulipwa kwa wale wanaosaidia katika zoezi la ukusanyaji wa mapato

Katibu Tawala alieleza kwamba hapo awali mapato yalikuwa chini na Mkurugenzi Mtendaji aliyehama Bw. Kevin S. Makonda aliweka mikakati mizuri ya ukusanyaji wa mapato, aidha alieleza kwamba kinachotakiwa ni kutoa ushauri wa nini kifanyike katika kuhakikisha mapato yanakusanywa pia kuziba mianya yote ambayo inaweza kupoteza mapato.

Mjumbe mwingine alisema kwamba Kata ya Kasulo malori ni mengi na yanaegeshwa nyakati za usiku, alishauri ili kuongeza mapato lile eneo ambalo Halmashauri ilinunua kwa ajili ya kuweka maegesho ya magari liboreshwe na kuanza kutumika kwa sababu mapato mengi yanapotea yanayotokana na ushuru wa maegesho ya magari

Mjumbe mwingine alisema kwamba ushuru wa forodha mipaka iwekwe vizuri ili ushuru uweze kukusanywa kwa sababu wanapofika kukusanya katika maeneo ya mipakani wanaelezwa kwamba eneo hilo sio la Halmashauri ya Wilaya ya Ngara, alishauri elimu kutolewa juu ya mipaka inayowekwa kwa sababu mapato ni mengi lakini yanapotea

Mweka hazina alisema kwamba kuhusu 10% kama Mtendaji wa kamata amewasilisha mapato na ikatokea kuna tatizo la kimtandao anatakiwa kuacha vielelezo vyake na kurudi siku nyingine na anakuta 10% yake.

Aidha alisema kwamba suala la vitabu vya kukusanyia ushuru vipo, kama Mtendaji atakosa awasiliane na Mweka hazina, aliomba ushirikiano pale inapotokea magari yanayobeba mizigo zaidi ya vibali wanavyopewa wabanwe na kulipia mizigo iliyozidi.

MAAZIMIO:

1. Mkurugenzi Mtendaji(W) afanye ufuatiliaji ili eneo lililonunuliwa na Halmashauri lililoko Benaco-Kasulo kujengwa eneo la maegesho ya magari ili kuongeza mapato ya Halmashauri
2. Iwekwe mikakati ya ukusanyaji wa mapato katika eneo la Kigoi-Nyakisasa ili mapato yaweze kukusanywa
3. Uwekwe utaratibu maalumu katika maeneo mbalimbali Wilayani ili kuwezesha waendesha bodaboda kulipia ushuru wa maegesho.

MUHT NA 8/2016/2017: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Afisa Mipango aliwasilisha taarifa na kufanya masahihisho na kueleza kuwa Halmashauri katika kipindi cha mwaka 2015/2016 iliidhinishiwa na Serikali kuu Tshs. 28,398,827,855/=, kama ifuatavyo Ruzuku ya mishahara Tshs. 19,754,132,000/=, Ruzuku ya matumizi mengineyo Tshs. 804,039,000/=, mapato kutokana na vyanzo vya Halmashauri Tshs. 1,682,110,000/= na Tshs. 4,158,546,855/= ikiwa ni fedha ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo toka Serikalini.

Halmashauri kufikia tarehe 30/06/2016 ilikuwa imepokea kiasi cha fedha Tshs. 29,632,054,798.62 sawa na 102.61% ya makisio ya mwaka.Mchanaganuo wa mapato hayo ni kama ifutavyo; Ruzuku ya mishahara Tshs. 22,175,319,551.97, Ruzuku ya matumizi mengineyo Tshs. 1,837,125,007.60/= na Tshs. 3,699,626,507.30/= ni bakaa ya miradi ya maendeleo.

Wajumbe walipokea taarifa na kuipitisha.

MUHT NA 9/2016/2017: MIKAKATI YA ULINZI NA USALAMA KATIKA WILAYA YA NGARA

OCD aliwasilisha taarifa kuwa mikakati ya Ulinzi na Usalama katika Wilaya ya Ngara;

HALI YA UJAMBAZI

Hali ya ujambazi wa kutumia silaha za moto(W) Ngara kwa kipindi cha mwezi January-September 2016 imeongezeka kwa 35% kulinganisha kipindi cha mwezi Januari mpaka Septemba. Asilimia 98%ujambazi huu unafanywa na raia toka nchi jirani ya Burundi ambao huingia vijiji vya mpakani jirani na nchi ya Burundi na kutekeleza uhalifu hii inatokana na kutapakaa kwa silaha za moto, kukosa hali ya utulivu wa kisiasa nchini Burundi na kusababisha hali ngumu ya maisha kwa kukosa chakula na njaa iliyoko nchini Burundi.

Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na;

- i. Polisi wa Ngara (W) kufanya doria/ misako katika maeneo mbalimbali yaliyopakana na nchi jirani ya Burundi kama vile Mugoma, Muruvyagira, Mabawe, Ibuga, D'Jululigwa, Mbuba, Kihinga, Mumilamila, Muganza, Keza, Magamba, Mikole na Mukalinzi
- ii. Kufanya doria barabara kuu Ngara-Rusumo-Nyakahura kwa kila siku za Jumanne na Alhamisi ili kuzuia utekaji unaofanywa na majambazi\
- iii. Polisi (W) Ngara imefungua kituo kidogo cha polisi maeneo ya Kijiji cha Mukalinzi-Murusagamba maalumu kwa ajili ya doria katika vijiji vya Mukalinzi, Magamba, Muganza na Murubanga.
- iv. Uimarishaji wa doria na misako maeneo yanayohudumiwa na vituo vidogo vya Polisi Mugoma, kabanga, Rulenge, Kasulo-Benako, Murusagamba na Rusumo Wananchi wana nafasi katika ulinzi kama vile vikundi vya ulinzi vijijini, utoaji wa taarifa za siri za wahalifu na uhalifu, kutoa ushirikiano kwa askari Polisi wanaofanya misako/doria kwenye maneo ya vijijini.

Changamoto wanazokutana nazo ni pamoja na uwazi wa mipaka na kuwepo kwa njia nyingi za panya, Watanzania/ wanakijiji waishio katika vijiji vya mipakani kuwaajiri wafanyakazi wa bei ya chini toka nchini Burundi kufanya kazi za ndani, kilimo, na kufuga mifugo, Uhaba wa mafuta ya magari ya Polisi kwa ajili ya kufanya doria katika maeneo tete, Wimbi la wakimbizi/wahamiaji haramu wengi kutoka nchini Burundi limeongezeka ambapo majambazi hujipenyeza na kuingia Tanzania

Ufumbuzi ni kupata ushirikiano toka kwa Polisi, Idara ya Uhamiaji-Ngara, Uongozi wa Vijiji/ Kata hasa Wenyeviti wa vijiji, Madiwani pia wasimamie wasiruhu mtu asiyejulikana anwani yake kufanya kazi zozote mpaka vyombo vya Usalama kujiridhisha. Wajumbe walipokea taarifa na kuijadili kama ifuatavyo;

Mjumbe mmoja alisema kwamba Kata ya Mabawe nayo inaathirika ns uvamizi wa ujio wa Warundi, alishauri vyombo vya usalama kuelekeza nguvu nyingi katika maeneo ya mipakani.

Mjumbe mwingine alishauri utaratibu wa daftari la usajili lirudishwe katika maeneo ya mipakani ili kupunguza ujio wa wakimbizi katika maeneo hayo kwa sababu itasaidia kuonesha mgeni aliyefika anatoka wapi na atakaa kwa muda gani.

Mjumbe mmoja alisema kwamba Kata ya Kirushya Kijiji cha Kasange kimekuwa na matukio ya uvamizi na kijiji hicho kipo karibu nan chi jirani ya Burundi, aliomba kuongezewa kituo cha Polisi ili kupunguza uhalifu.

Mjumbe mwingine alipendekeza kuwa ili kupunguza matukio ya kiuhalifu Wilaya ya Ngara iwekwe katika kanda maalumu na kuimarisha ulinzi wa Wilaya ya Ngara pia uwepo uwezekano wa upatikanaji wa gari la zima moto ili kusaidia katika majanga ya moto, aidha alieleza kwamba hapo awali kilifanyika kikao cha Wadau na azimio lililokuwa limetolewa ni kuanzisha mfuko wa Elimu wa Wilaya, alishauri mfuko wa Elimu wa Wilaya kurudishwa.

Mjumbe mmoja alisema kwamba Kata ya Mugoma ina vituo 2 vya Polisi na mara nyingi Watendaji wake (Polisi) wamekuwa wakihamishwa kila baada ya miezi 3, aliomba wanapofanya uhamisho Wakuu wa Vituo vya Polisi wasibadilishwe kwa sababu ya uzoefu pia kusaidia katika kudhibiti uvamizi wa Warundi.

Mwenyekiti wa Halmashauri alisema kwamba Mkuu wa Wilaya aangalie katika Mahakama za Mwanzo na hukumu zinazotolewa kwa wahalifu kwani ndogo sana ambapo wahalifu wanapotoka wanajigamba na kuendelea kufanya makosa, pia kumekuwa na tabia ya kukamata pikipiki hasa katika eneo la Kata ya Bugarama alitaka kufahamu fedha zinazotolewa na bodaboda kuwalipa Polisi zinawasilishwa wapi?.

Aidha aliomba ushirikiano wa Polisi na Halmashauri katika zoezi la ukusanyaji wa mapato kwa sababu Polisi wamekuwa wakizunguka na kushirikiana na Wafanyabiashara hasa kipindi cha mavuno ya Kahawa zimekuwa zikipitishwa bila kulipiwa ushuru.

Mjumbe mmoja alisema alishauri semina itolewe kwa waendesha pikipiki ili inapotokea wanafanya makosa watambue, pia Polisi wasaidie katika kuwakamata wahalifu na kuwaweka mahabusu.

Katibu Tawala(W) alisema kwamba katika maeneo ambayo ni hatarishi/ mipakani Polisi walishaenda kwa ajili ya ulinzi

Mjumbe mmoja alisema kwamba kama Halotel wanahitaji eneo kwa ajili ya kuweka minara waende Nyamagoma watapewa eneo hata pia Murusagamba.

OCD alisema kwamba suala la semina kuna Taasisi inaitwa REDESO ambayo inatoa mafunzo ya udereva, alishauri vijana wanaoendesha pikipiki kujikusanya na kujiunga kama kundi na kuwasiliana na ofisi ya OCD ili waweze kupatiwa semina

Aidha alisema kwamba kuhusiana na kesi zinazopelekwa Mahakamani, OCD alieleza kwamba ni jukumu la Polisi kupeleka kesi Mahakamani lakini hawawezi kuingilia taratibu za kimahakama, kuhusu wahalifu wanaokamatwa na kuachiliwa huru ni haki ya kila mtu kupata dhamana inategemeana na aina ya kosa alilofanya na jukumu la kutoa hukumu ni la Hakimu ila wahalifu wanapopatikana na hatia inakuwa ni ushindi kwa Polisi.

Askari wa Bugarama wanaokamata bodaboda OCD aliahidi kulifuatilia kwa ukaribu kushirikiana na kituo cha Polisi cha Rulenge, aidha aliongeza kwamba ajali za bodaboda zinaongezeka kwa kasi hivyo kama Polisi hawawezi kukaa kimya alishauri madereva wa bodaboda kutii sheria za barabarani bila shurti.

OCD alishauri pia kwamba ujenzi wa vituo vya Polisi ufanywe kwa nguvu za wananchi kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya pia wananchi waelimishwe na kuhimizwa katika masuala ya uzimaji wa moto.

Mwenyekiti alisema kwamba suala la ulinzi na usalama linaanzia nyumbani, wananchi wanatakiwa kuepukana na wahamiaji haramu na kuwafichua wale wote wanaohatarisha amani.

Katibu alisema kwamba Halmashauri ya Ngara haijakusanya fedha kutokana na mapato ya pikipiki, walipokuwa katika kikao TAMISEMI-DODOMA Waziri wa TAMISEMI alishauri na kuzitaka Halmashauri zote kusajili pikipiki zote na kuzipangia vituo ili kuweza kukusanya mapato kwa urahisi.

AZIMIO: Uongozi wa Kata/Kijiji kushirikiana na watu wa mitandao ya simu kama vile Halotel wasaidie kupatiwa eneo kwa ajili ya kuweka minara ili kurahisisha mawasiliano katika maeneo yaliyoko mipakani kama vile Kijiji cha Mukalinzi.

MUNT NA 10/2016/2017: MIKAKATI YA USAFI WA MAZINGIRA

Afisa Usafi na Mazingira aliwasilisha kuwa Mkoa wa Kagera kupitia kikao cha PHC kilichofanyika tarehe 29/04/2016 chini ya Mkuu wa Mkoa Major General Mstaafu Salumu Kijuu kiliteua siku ya Alhamisi kuwa siku ya kufanya na kusimamia shughuli za usafi wa mazingira katika Halmashauri zote za Mkoa wa Kagera.

Siku hiyo ya Alhamisi jamii nzima kwa ujumla inapaswa kujitokeza kufanya usafi wa mazingira katika maeneo yao kwa kufagia, kufyeka nyasi ndefu, kukusanya na kupeleka taka katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kuhifadhia taka (Vizimba). Shughuli hizi zote zitafanyika kuanzia saa 1.00 asubuhi mpaka saa 3.00 asubuhi

Watendaji wa Kata na Wataalam wengine ngazi ya Kata wanapaswa kuanisha maneneo ya kusimamia na kupanga utaratibu wa usimamizi kulingana na raslimali watu walioko katika Kata na kutoa taarifa ya utekelezaji kwa Mkurugenzi Mtendaji(W) kila wiki ya kwanza ya mwezi na kutoa mgawanyo wa maeneo ya uzimamizipamoja na wahusika watakaosimamia. Wajumbe walipokea taarifa na kuijadili kama ifuatavyo;

Katibu Tawala (W) alisema kwamba suala la usafi katika Halmashauri bado lipo nyuma sana pia mgawanyo wa maeneo ya kusimamia na wahusika waliopangwa ipo haja ya kuandaa mkakati upya.

Mjumbe mmoja aligusia juu ya changamoto ya taka zilizoko katika vizimba ambazo zisipotolewa kwa wakati huleta kero kwa wananchi na taka hizo huzalishwa kila siku, alishauri lipatikane eneo maalumu kwa ajili ya kutupa taka

Mjumbe mwingine alisema kwamba uwekwe mkakati mzuri juu ya usafi wa mazingira ili hata wananchi walioko vijijini waweze kushiriki katika suala la usafi kwa sababu kuna dhana imejengeka kuwa usafi unafanyika katika maeneo ya mjini tu.

Mjumbe mmoja alisema kwamba choo cha soko la Murunyinya hakijafunguliwa kwa zaidi ya miezi 6 suala hili linaleta adha kwa wananchi wanaoishi karibu na soko kwani wananchi wamekuwa wakijisaidia katika maeneo yanayozunguka soko na soko lina uwezo wa kubeba watu zaidi ya 500.

Afisa Usafi na Mazingira alisema kwamba Halmashauri imepata eneo kwa ajili ya kutupa takataka lakini bado halitatwaliwa rasmi, kuhusu choo cha soko la Murunyinya atawasiliana na Katibu wa Kamati ya Mazingira wa Kata ya Murukulazo kuona jinsi ya kutatua kero ya ukosefu wa huduma ya choo katika soko la Murunyinya ambacho kimefungwa.

AZIMIO: Afisa Usafi na Mazingira (W) Ngara afanye masahihisho kwenye mpango wa usimamizi wa usafi uliopo kwa kuhakikisha anapanga watu wanaoweza kusimamia maeneo ya usafi kikamilifu, mpango huo uguse vijiji vyote.

MUHT NA 11/2016/2017: UHIMIZAJI WANANCHI KUCHANGIA BIMA YA AFYA YA JAMII

Mganga Mkuu aliwasilisha taarifa yake kuwa Bima ya afya ya jamii (CHF) ni mfumo wa ulipiaji wa gharama za matibabu kabla ya mchangiaji kuugua, alieleza kwamba hadi kufikia Septemba 2016 hali ya uchangiaji wa mfuko wa Afya ya jamii katika Wilaya umeendelea kuimarika ambapo idadi ya kaya zinaendelea kuongezeka hadi kufikia kaya 7642 ambayo ni sawa na 12% ya lengo la kufikia kaya 63,293 zilizopo Wilayani.

Aidha alieleza faida za Bima ya Afya ya Jamii kuwa ni pamoja na kusaidia mgonjwa kupata huduma za Afya kwa gharama nafuu, kupata huduma ya matibabu kwa muda wa mwaka mzima kwa kutumia malipo aliyochangia, fedha zinazopatikana husaidia katika kuendesha kituo cha afya kama vile ununuzi wa vifaa tiba na kinga, kituo kupata fedha za tele kwa tele zaidi kwa ajili ya uendeshaji wa huduma za kituo

Njia za uhimizaji wananchi kuchangia Bima ya Afya ya Jamii ni pamoja na kutoa elimu kuhusu umuhimu wa Bima ya Afya kwa njia ya vyombo vya habari, kufanya uhamasishaji katika ngazi ya jamii kupitia mikutano ya hadhara, vikao vya WDC na VDC, kufanya usimamizi elekezi katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa kushirikiana na Waganga Wafawidhi wa vituo.

Wajumbe walipokea taarifa na kuijadili kama ifuatavyo;

Mjumbe mmoja alitaka kufahamu tofauti iliyopo kati ya CHF na NHIF

Mjumbe mwingine aligusia suala la upatikanaji wa dawa, hii ni kwa sababu wananchi wanalipia CHF lakini wanakosa huduma ya dawa, pia wanalipa Tshs. 10,000/= ya huduma ya CHF lakini hutozwa fedha kutokana na huduma waliyoipata jambo ambalo hukatisha tamaa.

Mjumbe mwingine aligusia suala la ucheleweshwaji wa kadi za Bima ya afya, kwani imekuwa ni tabia mwanachi kulipia huduma ya Bima ya afya lakini husubiri kadi kwa muda mrefu, pia kuna baadhi ya vituo vya afya havitoi risiti kwa wagonjwa

Mganga Mkuu alisema kwamba changamoto zipo lakini wananchi hawatakiwi kukata tama, kumekuwa na tatizo la upatikanaji wa dawa ila anaamini tatizo hilo litapungua kwa asilimia kubwa

Aidha alitoa ufafanuzi wa huduma za CHF kuwa wanachi hawawezi kwenda kutibiwa mahali pengine tofauti na pale walipoandikishwa, hii ni kwa sababu fedha za CHF huingizwa moja kwa moja kwenye akaunti ya kituo cha Afya husika na hakuna akaunti ya pamoja ya kukusanya pesa za CHF, alieleza pia kwamba tofauti na huduma za NHIF ambapo mwananchi anaweza kutibiwa katika hospitali yoyote ile. Tofauti nyingine ya huduma ya CHF ni kwamba mwanachi anachangia Tshs. 10,000/= kama gharama za matibabu kwa mwaka mzima na wanatibiwa watu 6 tu katika familia, ambapo huduma za NHIF Watumishi wanakatwa kila mwezi kupitia mishahara yao na ni huduma ya kitaifa.

Suala la ukosefu wa dawa Mganga Mkuu alisema kwamba ni tatizo la Kitaifa, Halmashauri imekuwa inatoa fedha na kuagiza dawa lakini dawa zinazoletwa zimekuwa ni pungufu, walishaomba mkopo wa Tshs. 100,000,000/= toka NHIF ili waweze kufungua duka la dawa la Wilaya katika Hospitali ya Nyamiaga, aidha alieleza kwamba kwa mwananchi anayelipia Bima ya Afya hatakiwi kulipa fedha kwa ajili ya kumuona daktari na kama inafanyika hivyo kinyume na utaratibu. Wagonjwa wafahamishwe kutoa taarifa iwapo tatizo hili linaendelea.

Suala la risiti za karatasi Kituo cha Afya Murusagamba Mganga Mkuu analifahamu, alieleza kwamba hiyo inatokana na Mganga Mkuu wa Kituo kudaiwa vitabu Halmashauri hivyo kushindwa kuchukua vitabu vingine, aliahidi kufuatilia suala hilo na kulifanyia kazi.

Mganga Mkuu alisema kwamba kuhusu ucheleweshwaji wa kadi za Bima ushauri umepokelewa na atafanya mawasiliano na Mkoani kuona namna ya kuzalisha kadi ambazo zinafanana na kadi za Bima kama wanavyofanya katika Wilaya ya Karagwe.

MUHT NA 12/2016/2017: TAARIFA YA SHUGHULI ZA MAENDELEO ZILIZOFANYWA NA NGO'S

Afisa Maendeleo ya Jamii aliwasilisha taarifa kama ifuatavyo; kushirikiana na Serikali, Mashirika yasiyo ya Kiserikali utoa mchango mkubwa katika kuhakikisha huduma za kijamii zinapatikana na kuwafikia wananchi. Katika kufanikisha hili shughuli au miradi mbalimbali ya maendeleo hutekelezwa katika maeneo na sekta mbalimbali ili kuhakikisha tunapata jamii bora yenye kupata yote mahitaji ya msingi na ziada.

Mashirika hayo hujishughulisha na kutoa elimu za masuala ya kisheria na kuandaa wasaidizi wa sheria kutoka katika Kata, kuangalia makundi hatarishi yaliyoko katika jamii kama vile watoto wanaoishi katika mazingira magumu, vijana na wazee na kuwasaidia katika kulipa karo za shule kwa wanafunzi, kutekeleza shughuli za kilimo.

Wajumbe walipokea taarifa na kuijadili.

Katibu Tawala(W) alishauri taarifa kuandaliwa kwa usahihi NGO's zitambulike na aina ya huduma zinazotolewa na NGO's katika Halmashauri ya Ngara.

MUHT NA 13/2016/2017: NAMNA YA KUTATUA MIGOGORO YA ARDHI

Afisa Ardhi na Maliasili aliwasilisha taarifa kama ifuatavyo, migogoro ya ardhi inasababishwa na ukosefu wa mpango wa matumizi bora ya ardhi, kugawa/kumilikisha ardhi bila kuzingatia mpango wa matumizi bora ya ardhi, ongezeko la watu, baadhi ya watu kutumia kwa ubinafsi maeneo yaliyohifadhiwa kisheria, viongozi kutumia madaraka yao vibaya katika kugawa ardhi za vijiji bila kushirikisha wananchi wote.

Utatuzi wa migogoro ya ardhi unaweza kufanyika kwa kushirikisha pande zote 2 zenye migogoro na msuluhishi asiyefungana na upande wowote pamoja na vielelezo vya mipaka kama ipo.

Vyombo ya utatuzi wa migogoro ni pamoja na

1. Baraza la Ardhi la Kijiji
2. Baraza la Ardhi la Kata
3. Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya

4. Mahakama kuu ya Rufaa ya Tanzania
Wajumbe walipokea taarifa na kuijadili.

Mjumbe mmoja alishauri kwamba Wajumbe wa Mabaraza la Kata kubadilishwa kwa sababu kuna Wajumbe ambao wapo katika Mabaraza lakini tayari walishafariki na Mabaraza yamekaa kwa muda mrefu, pia kuna baadhi ya wananchi hawafahamu Baraza la Ardhi lililopo Wilaya linafanya kazi gani kuna umuhimu Mwanasheria kutumia vyombo vya Habari kuwajulisha wananchi juu ya uwepo wa Baraza la Ardhi la Wilaya, pia itafutwe namna ya kurudisha kesi zilizofunguliwa Chato na kurudishwa Ngara.

Mwenyekiti wa Halmashauri alishauri juu ya utengenezaji wa ardhi katika eneo la hifadhi. Hii ni kwa sababu hakuna wanyama katika hifadhi hiyo na kuweka ardhi inaweza kusaidia Halmashauri katika suala la migogoro ya ardhi hasa katika Kata ya Kasulo hivyo ofisi ya ardhi iangalie suala hili kwa makini.

Mjumbe mwingine alichangia kuhusu uwezeshwaji wa Baraza ya Kata kwa sababu Wajumbe wa Mabaraza ya Kata hawana uelewa juu ya sheria ndogo za ardhi jambo ambalo linapelekea kushindwa kutatua migogoro, alishauri Mabaraza hayo kuwezeshwa kifedha ili yaweze kujiendesha kikamilifu.

Mjumbe mmoja alishauri maeneo yote kupimwa na kusajili ili yaweze kupata hati na kutambuliwa.

Afisa Ardhi na Maliasili alisema kwamba suala la kubadilisha Wajumbe walioko katika Mabaraza ya Kata litazingatiwa kwa kushirikiana na Mwanasheria, pia suala la kuwajulisha wananchi kuhusu Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya atawasiliana na Mwanasheria ili aweze kulifanyia kazi.

Aidha alieleza kwamba kuhusu mgogoro wa ardhi uliopo Kasulo kati ya Masista wa Kanisa Katoliki na wananchi mgogoro huo ni rahisi kusuluhisha kwa sababu tayari masista wana ramani hivyo ofisi ya ardhi itafika baada ya kupata vielelezo na kupima na kuweka mipaka na kuweza kutatua mgogoro huo.

Suala la kujengea uwezo mabaraza ya radhi, Afisa Ardhi na Maliasili alieleza kwamba atalitaftua utatuzi kwa kushirikiana na Mwanasheria na kuhusu umiliki wa maeneo ya mabondeni Mhandisi wa Maji aleleza kwamba ipo sheria inayoeleza kwamba maeneo yote ambayo yana vyanzo vya maji yanatakiwa kuachwa mita 60 kila upande kutoka katika chanzo cha maji.

Aidha alieleza kwamba suala la kutopima vijiji na kuweza kutambulika, changamoto iliyopo ni ukosefu wa fedha kwa ajili ya zoezi la upimaji wa ardhi, pia alieleza kwamba suala la umiliki wa ardhi inategemea na aina ya umiliki ambayo mwananchi anakuwa amepatiwa katika hati kuna umiliki wa miaka 99 na 33 na pia upo umiliki kwa kutumia hati za kimila ambapo umiliki huu unakuwa ni wa kudumu kama inatokea mmiliki hajaendeleza eneo analomiliki kwa muda wa miaka 5 na kuendelea anaweza kufutiwa hati ya umiliki kwa kushindwa kuendeleza eneo.

AZIMIO: Mkurugenzi Mtendaji (W) afanye ufuatiliaji na kubaini Mabaraza ya Kata ambayo yameshapitwa na muda wake ili yaundwe upya na Wajumbe wa Mabaraza wapewe elimu kuhusu majukumu yao.

MUHT NA 14/2016/2017: KUFUNGA KIKAO

Katib aliwashukuru Wajumbe kwa kuweza kuhudhuria kikao na michango yoyeiliyotolewa katika agenda zilizowasilishwa ambayo inaweza kuleta tija na kumkaribisha Katibu Tawala aweze kumkaribisha Mwenyekiti aweze kufunga kikao.

Mwenyekiti alisema kwamba yale yote yaliyo chini ya uwezo wa Halmashauri yasimamiwe na kufanyiwa kazi nay ale yaliyo juu ya uwezo wa Halmashauri yatawasilishwa katika ngazi za juu aliwashukuru wajumbe kwa kuhudhuria kikao. Kikao kilifungwa saa 11.00 jioni.

UMETHIBITISHWA

.....
Mh. LT CLO MICHAEL MNJENJELE
MWENYEKITI

.....
Bw. AIDAN J. BAHAMA
KATIBU

Tarehe...../.....2016

MUHTASARI WA MAAZIMIO NA HATUA ZA UTEKELEZAJI WA KIKAO CHA

DCC KILICHOFANYIKA TAREHE 03/10/2016

MUHT.NA	MAAZIMIO	MHUSIKA	HATUA ZA UTEKELEZAJI
MUHT NA 4/2016/2017	HALI YA UTENGENEZAJI WA MADAWATI Wajumbe waliazimia kwamba Afisa Elimu Msingi asimamie na kufuatilia waraka wa usimamizi wa elimu ngazi ya kata	DED/DPEO	
	Wajumbe waliazimia kwamba Mkurugenzi Mtendaji afuatilie ahadi iliyotolewa na Benki ya NMB na majibu yatakayotolewa na Benki ya NMB yawasilishwe kwa Mwenyekiti wa Halmashauri na taarifa itatolewa kupitia vikao vya Halmashauri.	DED	
5/2016/2017	MIKKATI YA KUONDOA WATUMISHI HEWA Wajumbe waliazimia kwamba Afisa Elimu Msingi na Afisa Elimu Sekondari wafuatilie ili kbaini wanafunzi hewa na kutoa taarifa kwa Mkuu wa Wilaya kwa ajili ya kuchukua hatua.	DED/DPEO	
	Wajumbe waliazimia kwamba Afisa Elimu Msingi na Afisa Elimu Sekondari wafuatilie ili wajumbe wa Bodi waliomaliza muda wao wachaguliwe wengine aidha vikao vya Bodi vifanyike kulingana na maelekezo yaliyopo.	DPEO/DSEO	

6/2016/2017	<p>MAANDALIZI YA MISIMU YA KILIMO</p> <p>Wajumbe waliazimia kwamba Kikao cha DCC Ngara kinaomba kupitia kikao cha kinachofuata kufuatilia suala la pembejeo za kilimo kuletwa kwa wakati kwa wakulima kulingana na misimu ya kilimo iliyoko katika Wilaya ya Ngara kuanzia mwezi Julai kila mwaka.</p>	DC/DED/DAICO	
	<p>Wajumbe waliazimia kwamba Afisa Kilimo awaagize Maafisa Kilimo kuondoka maofisini na kwenda kwa wananchi ili kutoa ushauri, maelekezo na Teknolojia mpya ya kilimo.</p>	DAICO	
<p>MUHT NA 7/2016/2017</p>	<p>MIKAKATI YA MAKUSANYO YA NDANI</p> <p>Mkurugenzi Mtendaji(W) afanye ufuatiliaji ili eneo lililonunuliwa na Halmashauri lililoko Benaco-Kasulo kujengwa eneo la maegesho ya magari ili kuongeza mapato ya Halmashauri</p>	DED/DT	
	<p>Wajumbe waliazimia kwamba iwekwe mikakati ya ukusanyaji wa mapato katika eneo la Kigoi-Nyakisasa ili mapato yaweze kukusanywa</p>	DED/DT	
	<p>Wajumbe waliazimia kwamba Uwekwe utaratibu maalumu katika maeneo mbalimbali Wilayani ili kuwezesha waendesha bodaboda kulipia</p>	DED/DT	

	ushuru wa maegesho.		
9/2016/2017	<p>MIKAKATI YA ULINZI NA USALAMA</p> <p>Wajumbe waliazimia kwamba Uongozi wa Kata/Kijiji kushirikiana na watu wa mitandao ya simu kama vile Halotel wasaidie kupatiwa eneo kwa ajili ya kuweka minara ili kurahisisha mawasiliano katika maeneo yaliyoko mipakani kama vile Kijiji cha Mukalinzi.</p>	DED/OCD	
	<p>Wajumbe waliazimia kwamba Mkurugenzi Mtendaji (W) afanye ufuatiliaji na kubaini Mabaraza ya Kata ambayo yameshapitwa na muda wake ili yaundwe upya na Wajumbe wa Mabaraza wapewe elimu kuhusu majukumu yao.</p>	DED/LO	